



## Mmbora wenu ni yule aliyejifunza Qur'ani na akaifundisha

Imepokewa kutoka kwa Othman -Radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Mmbora wenu ni yule aliyejifunza Qur'ani na akaifundisha".

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Anaeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- yakuwa muislamu bora na aliye na daraja ya juu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu: Ni yule aliyejifunza Qur'ani, kwa kuisoma na kuihifadhi na kuisoma vizuri na kuiielewa na kuitafsiri, na akamfundisha mwingine kile alichonacho katika elimu za Qur'ani pamoja na kuifanyia kazi.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/5913>

النجاة الخيرية  
ALNAJAT CHARITY

